
HISTORIA YA KARISMATIKI KATOLIKI
PAPA YOHANE XXIII
1958 - 1963
PAPA LEO XIII
1878 - 1903
PAPA PAULO VI
1963 - 1978
SR. ELENA GUERA
1835 - 1914
PAPA YOHANE PAULO II
1978 - 2005
Imeandikwa na:
Fr. Pius Shao na Benedict Mwakyanjala
Agape Publications

# HISTORIA YA KARISMATIKI KATOLIKI

## KARISMATIKI KATOLIKI

## TUMAINI LA KANISA MILLENNIA YA TATU

Kiliandikwa na

FR. Pius Shao na Benedict Mwakyanjala

Kipigo chapa cha Mtandao
2024

**ISBN 9789912420328**

**Agape Publications**
**P.O.Box 76021 Dar-es-Salaam**
**Simu : + 255 767 342068**
e-mail : kungweformat@gmail.com

# YALIYOMO

DIBAJI uk. 4

Roman Lyimo
Agape Centre

UTANGULIZI uk. 10

SEHEMU YA KWANZA uk 12

Maana, Uwepo na historia ya Karismatiki Katoliki.

Fr; Pius Shao

SEHEMU YA PILI uk. 38

Historia ya Upyaisho wa Kikarismatiki Katoliki

Ilivyoingia Tanzania.

Benedikto Mwakyanjala

# DIBAJI

Upyaisho wa Kikarama katika Kanisa Katoliki umekuja kadiri ya mpango wa Mungu na utendaji wa Roho Mtakatifu wakati muafaka, wakati ambao kweli ulihitajika. Mtu mmoja aliniuliza ,"Hivi kama si Upyaisho huu uliokuja karibu miaka 48 iliyopita hali yetu ingekuwaje hivi sasa?" Ni kweli. Upyaisho huu umeleta uhai katika nyanja nyingi za Kanisa na Imani na kwa walioukumbatia, maisha yao kiroho, kinafsi na kimwili yamebadilika. Ni furaha iliyoje kuonja utendaji ule ule wa Roho Mtakatifu wakati wa Matendo ya Mitume wakati wetu huu kwa namna y kutia moyo sana.

Katika hotuba yake kwa Halmashauri Kuu ya Upyaisho wa Kikarama kaiika Kanisa Katoliki, (*Catholic Charismatic Renewal*) kwa maneno mengine Karismatiki Katoliki ilipotimiza miaka 25 ulimwenwi huko Roma tarehe 14 Machi, 1992, Papa Yohane Paulo II alisema: "Katika mwisho huu wa miaka 2000, Kanisa linahitaji zaidi kumgeukia kwa uhakika na matumaini, Roho Mtakatifu ambaye bila kuchoka anawavuta waamini katika Ushirika wa Upendo wa Utatu akishikamanisha upendo wao katika mwili mmoja wa Kristo, na kuwatuma kwa ajili ya huduma ya Kitume iliyokabidhiwa kwa Mitume na Yesu Mfufuka. Ni lazima tushawishiwe kuwa ufahamu wa ndani zaidi wa Nafsi na kazi ya Roho Mtakatifu unawiana na mahitaji ya nyakati zetu, kwani Roho Mtakatifu yuko katikati ya Imani ya Mkristo na Ndiye chanzo cha nguvu ya

mabadiliko ya Kanisa" (*Dominum et Vivificatem*, 2). Ni kweli kabisa kuwa Roho Mtakatifu Ndiye Mtendaji Mkuu wa Huduma ya Kanisa (*Redemptoris Missio*, 21) anayekulinda na kuimarisha. Juhudi zote Kanisani za kuwaletea watu wote neema ya Pentekoste... Wakati huu katika historia ya Kanisa, Uamsho wa Roho Mtakatifu unaweza kutenda jambo muhimu katika kulinda Imani ya Kikristo katilca.jamii, ambayo vitu vya kidunia vimedhoofisha Inani ya wengi na hivyo kushindwa. kumtii Roho Mtakatifu na kuutambua mwito wa upendo wa Mungu Mchango wenu katika kufanya Uinjilishaji mpya unaweza kufanywa kwa ushuhuda wa binafsi kwa njia ya Roho akaaye ndani na kwa kuonesha uwepo wake kwa matendo ya Utakatifu na mshikamano. Ushuhuda wa maisha ya Mkristo ni njia ya kwanza isiyoweza kuchukuliwa na nyingine katika huduma (*Redemptoris Missio*, 42). Ni njia gani nyingine iliyopo ya kuweza kuwavuta watu waliopoteza juhudi za kiroho za ukweli huo ambao peke yake unaweza kutuliza moyo wa mwanadamu ulio na mahangaiko mengi. Hakuna njia nyingine isipokuwa ni ya maisha ya Wakristo walio na Imani thabiti. Kuwa mashahidi ni kuwa chachu yenye nguvu kati ya watu ambao hawajafahamu kabisa thamani ya wokovu ambao Yesu peke yake ndiye mwenye kuutoa."

Wakati wa Mkutano wa kwanza wa Kimataifa wa Viongozi wa Karismatiki Katoliki, tarehe 1 0ktoba 1973,'Papa Paulo VI alisema, "Tunashangilia pamoja nanyi, wapendwa marafiki kktika Upyaisho wa maisha ya kiroho yanayojidhihirisha katika Kanisa siku hizi, kwa namna mbalimbali na katika mazingira mbalimbali. Kuna mambo yana rofanana kote yanayotokea katika

Upyaisho huu muonjo wa sala za kina, za mtu binafsi na kwa makundi, kurejea kwa taamuli na msisitizo wa Sifa za Mungu, tamanio la mtu kujiachilia kwa Kristo, uwepo wa hali ya juu wa mwitikio kwa miito ya Roho Mtakatifu, usomaji wa Maandiko Matakatifu kwa uangalifu zaidi, ukarimu wa kujitoa kindugu, ukubali wa kuchangia huduma za Kanisa. Katika haya yote, tunaweza kutambua miujiza, maftmbo na umakini wa utendaji wa Roho Mtakatifu, ambaye ni Moyo wa Kanisa."

Mwaka 1975, Papa Paulo VI mwenyewe binafsi alialika Karismatiki Katoliki kufanya Mkutano wao wa imataifa huko Roma. Katika kipindi maalum wakati wa Mkutano ule Papa alitamka"Mmechagua Jiji la Roma katika mwaka huu Mtakatifu kusherekea Mkutano wenu wa Kimataifa, wapendwa wanangu wa kiume na wa kike ; mmetuomba tukutane nanyi leo na kuwahutubia. Mmetamani kwa jinsi hiyo kuonesha kuambatana kwenu na Kanisa lililoanzishwa na Yesu Kristo na kwa kila kitu ambacho Kiti hiki cha Petro kinawakilisha kwenu. Tamanio lenu hili kubwa la kujishirikisha · ndani ya Kanisa ni ishara thabiti na ya kweli ya utendaji wa Roho Mtakatifu.

Kama tulivyosema mwezi Oktoba na baadhi yenu mkiwepo, Kanisa na Ulimwengu vinahitaji sasa kuliko wakati wowote mwingine kwamba mwujiza wa pentekoste uendelee katika historia... Hakuna lililo la muhimu zaidi katika ulimwengu huu unaoendeshwa na malimwengu zaidi kuliko ushuhuda wa "Upyaisho wa kiroho" ambao tunaona Roho Mtakatifu akiamsha katika

maeneo mbalimbali na mazingira mbalimbali... Ni kwa nini sasa "Upyaisho huu wa kiroho" usiwe "fursa" "na bahati njema" kwa Kanisa na kwa Ulimwengu? Na kwa nini kama ni hivyo, kila mtu asichukue njia zote za kuhakikisha kwamba inabakia hivyo?"

Katika Mkutano wa Kimataifa wa Karismatiki Katoliki 1979, Papa Yohane Paulo II alisema "Daima nimekuwa katika Upyaisho huu katika Roho Mtakatifu. Uzoefu wangu binafsi unapendeza sana. Nilipokuwa Shuleni kati ya umri wa miaka 12 au 13, mara kwa mara nilipata matatizo katika masomo yangu, hasa katika Hisabati. Baba yangu akanipa kitabu cha sala. Akakifungua ukurasa fulani na akaniambia "Hapa kuna sala kwa Roho Mtakatifu. Lazima usali sala hii kila siku katika maisha yako": Nimedumu katika utii kwa sala hiyo ambayo Baba yangu alinipa miaka 50 iliyopita... Nathibitisha kuwa mkondo huu (Karismatiki Katoliki) ni ishara ya utendaji wake. Ulimwengu unahitaji sana utendaji huu wa Roho Mtakatifu, na utendaji huu unahitaji vyombo vingi sana. Hali katika ulimwengu ni ya hatari, ya hatari sana. Malimwengu yanapingana na ukweli halisi wa nguvu za mwanadamu, na kuna malimwengu aina nyingi. Malimwengu ni kukana Roho Mtakatifu. Sasa nauona mkondo huu, utendaji huu kila mahali... Na hivyo hivyo inanithibitishia Upyaisho wa Kanisa zima, katika Upyaisho huu wa kiroho wa Kanisa. "

Papa Benedict XVI wakati akiwa Kardinali Joseph Ratzinger, katika mahojiano na Ignatius Press, 1985 alisema "Ambalo ni matumaini katika ngazi ya Kanisa la Ulimwengu na kinachotokea ndani kabisa ya moyo

wa msukosuko wa Kanisa la ulimwengu wa Magharibi ni kukua kwa mikondo mipya ambayo haikupangwa na yeyote, na ambayo uwepo wake haukuitwa na yeyote, lakini ambayo imechipuka yenyewe. Kinachojitokeza katika mikondo hii ingawa kimetiishwa/kimewekewa utaratibu ni kitu kama msimu wa Pentekoste katika Kanisa. Nafikiria kuhusu, kama mkondo huu wa Karismatiki, wa Kursillo....

Furaha ya Imani ambayo mtu anakutana nayo hapa ina kitu cha kuambukizana ndani yake. Hapa miito mipya ya Upadre na Utawa inakua … Kinachojitokeza ni kizazi kipya cha Kanisa ambacho nakiangalia kwa matumaini makuu. Naona ni ajabu kwamba Roho Mtakatifu kwa mara nyingine tena ana nguvu kuliko programu zetu na anajileta mwenyewe kwenye mchezo kwa njia tofauti kabisa kuliko tulivyofikiria. Kwa namna hii, Upyaisho katika hali ya kutiishwa au kuthibitiwa hata hivyo ni njia yenye matokeo mazuri, ni mguu wa kuknyagia.... "
Akihutubia mkutano mkubwa wa Wanakarismatiki katika uwanja mkubwa wa michezo (*Stadium*) mjini Roma mwezi June 2014 Papa Francis alisema "Ninapowafikiria Wanakarismatiki nalifikiria Kanisa lenyewe, lakini kwa namna ya pekee nafikiria bendi kubwa ya muziki ambapo vyombo mbalimbali vyenye sauti mbalimbali huwekwa pamoja ili kuufanya muziki upendeze. Mtume Paulo anaongelea hiti katika Barua yake ya kwanza kwa Wakorintho sura ya 12 kuhusu karama mbalimbali, lakini Roho ni yule yule.... "
Kama mjuavyo-kwa sababu habari husambaa haraka sana-katika miaka ya kwanza ya Karismatiki Katoliki huko Buenes Aires Argentina, sikuwajali sana

Wakarismatiki. Nilikuwa nafikiri; "Wananigonga kama aina fulani ya shule ya Samba': Sikushiriki mtindo wao wa sala au mambo mengine mengi mapya yaliyokuwa yanatokea katika Kanisa. Baadae, nilikuja wafahamu, na hatimae nikagundua mazuri yote ambayo Upyaisho wa Karama (au Karismatiki Katoliki) uliyokuwa unafanya kwa ajili ya Kanisa. Na ile hadithi iliyoanza na "shule ya Samba" iliishia bila kutarajia.Miezi michache kabla ya kuingia kwenye Baraza la siri la Makardinali linalomchagua Papa nilitajwa kuwa msaidizi wa kiroho wa Karismatiki Katoliki kule Argentina na Baraza la Maaskofu.
Karismatiki Katoliki ni nguvu kubwa inayodhamiria kuhudumu kwa kuhubiri Injili katika furaha ya Roho Mtakatifu.... "

Roman Lyimo,
Agape Centre,
Dar es Salaam.

# UTANGULIZI

Mkondo wa Karismatiki Katolil«i ulianza mwaka 1967, yaani miaka miwili tu baada ya kufungwa kwa Mtanguzo Mkuu wa Piti wa Vatikani. Kwa miaka minane tu mfumo huo ulienea upesi mno na kutapakaa karibu nchi zote ulimwenguni. Katika kuenea huko, kuna ushahidi mahttsusi kwamba ulitapakaa wenyewe ukianzishwa katika nchi mbali mbali bila kuratibishwa, kupangiliwa au kuhamasishwa na vikundi vilivyokwisha kuanzishwa tayari katika nchi nyingine. Hata hivyo mfumo huo katika Kanisa Katoliki unabainishwa karibu kila mahali na alama zinazofanana

* Ari ya sala za peke peke na za vikundi.
* Mkazo katika sala za masifu na kuabudu.
* Mvuto wa kujiachilia kabisa kwa Kristu.
* Utayari wa kuitikia mwito wa Roho Mtakatifu.
* Njaa na kiu ya kusoma neno la Mungu.
* Majitoleo makubwa kutekeleza upendo wa kindugu.
* Kujitolea kwa ajili ya utumishi wa Kanisa.
* Ari kubwa sana ya kuinjilisha.
* Mwto mkubwa kwa ajih ya maombezi.

**Swali ni**:

Je inawezakana kwamba mfumo huu ni jibu kwa ile sala ya Baba Mtakatifu Yohane XXIII ya kuita Mtaguzo wa piti wa Vatiliani? Alisali kuombea ili kuweko maajabu kama ya Pentekoste mpya katika nyakati zetu. Je huu mfumo wa Karismatiki Katoliki katika Kanisa ni

matokeo ya Mtaguso huo Mkuu wa Pili wa Vatikani? Lengo lake lilikuwa kufanya upya Kanisa zima kuendana na alama za nyakati.
Je mfumo huu ni wa mpito au ni wa kudumu? Unagusa k wa undani kiasi gani asili na muundo wa Jumuiya ya Kanisa? Jc tunaweza kusema kwa hakika kwamba mfumo wa Karismatiki Katoliki ndilo tumaini la Kanisa kwa siku za usoni?

1li kujadili kinaganaga na kikamilifu maswali hayo tutachunguza mfumo huo wa Karismatiki katika fani hizi

* Uwepo wa Karismatiki Katoliki katika Kanisa Katoliki
* Maana ya Karismatil«i Katoli]«i
* Malengo ya Karismatiki Katoliki
* Historia ya Karismatiki Katoliki
* Nguzo zake:
    - Kuongoka na kujiachia kabisa kwa Yesu
    - Ubatizo katika Roho Mtakatifu
    - Uinjilishaji Mpya
* Machimbuko
    - Katika utume wa Yesu.
    - Katika maandiko Matakatifu
    - Katika Mangmuzi ya Mtaguso wa piti wa Vatikani.

Kudodosa ni kwa namna gani na kwa kiasi gani tunaweza kusema kwamba mfumo huu wa Karismatiki Katoliki ndilo tumaini la Kanisa Katoliki kwa siku za usoni?

# SEHEMU YA KWANZA

## 1. 1 MAANA, UWEPO NA HISTORIA YA KARISMATIKI KATOLIKI.

Mfumo wa Karismatiki Katoliki ulianza Mjini Pittsburg Marekani mwaka 1967 wakati wa Mafungo ya wanachuo na Maprofesa wa -Chuo Kikuu cha Duquesne walipopata ujazo mpya wa Roho Mtakatifu. Ujazo huu ulibadilisha kimsingi maisha yao. Kabla ya hapo wanachuo hao walikuwa wametambua peke peke kwamba ingawaje walimfahamu Kristu na ingawaje walimthamini sana katika maisha yao, hata hivyo Kristu hakuwa kweli ndiye mnsingi wa maisha na mipango yao. Kita mmoja alijisikia hitaji kubwa la kujiachilia kabisa kwa Kristu. Walitafuta namna ya kufanya hivyo katika kusoma maaandiko Matakatifu, hasa Matendo ya Mitume kwa undani zaidi katika kusali peke peke na kama kikundi na katika hayo mafungo. Matokeo ya jitihada zote hizi ni huo mmiminiko mpya wa Roho Mtakatifu waliokuwa wanatamani.

Tukio hiti limejirudia katika sehemu mbali mbali za dunia na kuleta matokeo yanayofanana yaani ishara, maajabu, na Karama mithili ya zile za Pentekoste ya mwanzo. Kinachoonekana wazi katika Vikundi vyote vilivyopatwa na tukio hiti ni kwamba kuna kuweko na amani ya pekee ya ndani na mabadiliko makubwa ya maisha kwa Kiyunani *Metanoia*, na kujitokeza kwa karama mbali mbali. Mftuno huu unaojidhihirisha katika Kanisa Katohki baada ya Mtaguso wa pili wa Vatikani, ndio unaojulikana kama Karismatiki Katoliki. Ni

kufanywa upya katika Kanisa kwa mwamsho wa Karama za Roho Mtakatifu.

Inavyoonekana ni kwamba tengo la mfumo huu wa Karismatiki ni kufanya upya umbile lote la Kanisa kwa mabadiliko ya kina ambayo yanafurikia katika muundo wake wa kijamii na Taasisi zake. Hivyo vikundi vinaundwa na watu wa miito mbali mbali i. e. Maaskofu, Mapadre, watawa na walei. Pia vikundi vinajumuisha watu wa umri tofauti, jinsia na hali mbali mbali za maisha. Kutokana na hali hii tunaweza kusema kwamba mabadiliko haya ya Karismatiki yanagusa kwa undani asili na muundo wa Kanisa. Mfumo unachimbuka ndani ya Kanisa, unajidhihirisha katika Kanisa na tutaona kama kweli ni kwa manufaa ya Kanisa,

Kama mkondo huu unavyojionyesha, ni ishara kamili ya uwepo wa Roho Mtakatifu akifanya kazi katika Kanisa. Kwa kusema hivi sina maana kwamba kazi ya Roho Mtakatifu katika Kanisa imeanza tu na huu mfurno wa Karismatiki. La hasha. Roho Mtakatifu ndiye aliyekabidhiwa na Yesu Kazi ya kuliunda Kanisa. Aliwaagiza wafuasi wake akisema "*Nami mwenyewe nitawapelekeeni Yule ambaye Baba Aliahidi kumtuma, lakini ngojeni huku mjini mpaka mtakapopewa ile nguvu itokayo juu*" Lk 2449. Hayo yalitimia wakati wa Pentekoste ya kwanza. Roho Mtakatifu aliwashukia wafuasi na kuliunda Kanisa yaani familia ya Kristo ya wale wanaomwamini au mwili mfumbwa wa Kristo. Hivyo ndivyo alivyoshuhudia Mt. Petro katika mahubiri yake siku ile ya Pentekoste ya kwanza. "*Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate*

*ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadihii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.... Nao waliohpokea neno lake wakabatizwa na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu*" Mdo 2:38-39, 41. Ni Roho Mtakatifu aliyewaunda hao pamoja. Tangu wakati huo anaendelea kutenda kazi, kwani ndivyo Yesu alivyoahidi."*Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele ndiye Roho wa kweli, ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye. Atakuwa ndani yenu:* " Yn.14:16-17.

Hakika Roho Mtakatifu anatenda kazi kwa kudumu katika Kanisa, Amedhihirisha uwepo wake kwa uwazi zaidi katika nyakati mbali mbali za mabadiliko makubwa. Kwa mfano katika kuanzisha mashirika mbali mbali ya kitawa ili kuishi karama na mausia ya kienjili kwa ajili ya kuboresha Kanisa. Mtakatifu Francis wa Asisi kwa mfano aliweza tu kuzingatia ufukara kamili na kujikusanyia Ndugu waliotaka kuishi Karama hiyo kutokana na uvuvio wa Roho Mtakatifu. Au Mtakatifu Benedikti. Yeye aliona umuhimu wa kuunganisha Sala na kazi na kutunga mwongozo wa utawa wa kuishi hayo mawili. Ni Roho Mtakatifu aliyemwongoza kufanya hivyo. Kwa hivyo Roho Mtakatifu alikuwa kazini katika kulihuisha Kanisa nyakati zote. Pia wakati wa madhulumu ya Kanisa, Roho Mtakatifu amewaimarisha waamini hata wakawa tayari kutoa maisha yao kwa ajili

ya kumshuhudia Kristo. Kristo mweyewe alitangulia kuwaasa wafuasi wake akisema: "*Lakini mtapokea nguvu, akisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi w o te, na Samaria, na hata Mwisho wa nchi.* " Mdo. 1 8. Roho Mtatifu amekuwa mwaminifu katika kulisimamia na kuliongoza Kanisa nyakati zote. Lakini hiki tunachoona sasa katika Karismatiki Katoliki ni tofauti. Huu mwamko unaoonekana baada ya Mtaguso wa Vatikani wa Pili na unaotikisa Kanisa zima, unatokana na Mtaguso huo na umezuka kama Upyaisho wa Karama za Roho Mtakatifu katika Kanisa.

Kuhitimisha sehemu hii, tunaweza kusema kwa usahihi kwamba, "Upyaisho wa Karismatiki Katoliki ni kielelezo au dhihirisho la mfumo unaotoka kwa Mwenyezi Mungu kwa tengo la kufanya upya Kanisa lote kwa mwamsho wa Karama yaani kufanya upya Kanisa katika ngazi zote za maisha yake kwa ujazo wa paji la Roho Mtakatifu, mapaji na huduma za Roho Mtakatifu "Kwa hiyo upyaisho wa Karismatiki Katoliki sio tu mtikiso katika Kanisa Katoliki, bali ni Kanisa lenyewe kama Jumuiya hai katika mabadiliko yake mithili ya kiumbe kilicho hai.

## **1. 2 MAANA YA KARISMATIKI KATOLIKI**.

Ni mkondo wa neema uliobubujika kutoka Mtaguso wa Vatikani wa pili unaowawta wankanisa wote warudie kwenye msingi wa Ubatizo wao na kuonja ukombozi wa binafsi unaoletwa na Yesu ambaye ni Bwana na Mwokozi pekee wa ulimwengu wote. Mkondo huu unawviwa na Roho Mtakatifu ambaye ndiye aliyepewa

jukumu la kumshuhudia Mistu, yaani kutakatifuza, kuongoza, kufundisha, kukumbusha, kuamsha, kuchochea karama n. k.

Mkondo huu unaitwa Upyaisho kwa sababu unalenga kurudia kwenye misingi ya unyago wa Kikristu yaani, ubatizo katika Roho Mtakatifu. unaitwa pia Uanusho kutokana na mbububujiko wa karama za Roho Mtakatifu zinazojitokeza katika huo Upyaisho.

Ni wazi kwamba Yesu ndiye chanzo cha neema zote. "*Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa mwana pekee atokalye kwa Baba amejaa neema na kweli*" Yn. 1:14 na pia mahali pengine, "*Kwa kuwa katika utinilifu wake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema. Kwa kuwa Torati ilitolewa kwa mkono wa Musa neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristu*. " Yn. 16-17. Naam, Yesu ametumwa na Baba kutudhihirishia Upendo wake na kutushirikisha uwana pamoja naye. "*Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu.* " Yn. 112.

Ni wazi pia kwamba yeye ndiye pekee chanzo cha wokovu wetu.-"*Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu, ambaye alijitoa mwenycwe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote, utakaoshuhudiwa kwa majira yake*" 1 Tim. 2;5-6. Lakini Roho Mtakatifu ndiye anayetuvuta tuingie katika usharika na Baba na Mwana. "*Kwa kuwa hamkupokea tena roho ya utumwa iletayo hofu*

*bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia,-Abba' yaani 'Baba'*" Rum. 815 na mahali pengine, "*Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya Sheria, kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hall ya kuwa wana. Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliayc, Abba! yaani,'Baba! : Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu.* " 'Gal. 44-7.

Kwa hiyo ingawaje huu mkondo wa neema ni kazi ya Nafsi zote za Utatu Mtakatifu, hata hivyo tunamwona Roho Mtakatifu akiwa ndiye Mtendaji zaidi wa huu upyaisho. Hii ndio maana tunapozungumza mara kwa mara juu ya Karismatiki Katoliki tunahusisha na Pentokoste Mpya. Wakati mwingine tunapozungum za juu ya Karismatiki Katoliki na kusisitiza kazi ya Roho Mtakatifu tunazungumzia zaidi juu ya Ubatizo katika Roho Mtakatifu tukiwa tunalenga zaidi hali hiyo anayoonja muumini yule anayejiachia kabisa kwa Yesu kama Bwana na Mwokozi wake baada ya Semina ya maisha ya Kiroho na jinsi anavyopata miminiko jipya la Roho Mtakatifu kama vile ni ubatizo. Hali hiyo ilikuwa ya kawaida kabisa katika ubatizo wakati wa Kanisa la mwanzo. Pia ilienda sambamba na ahadi ya Yesu, "*Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba,'ile ambayo mlisikia habari zake kwangu ya kwamba Yohane alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache.* " Mdo. 1 4-5.

Tunaweza kusema kwa kifupi kwamba Karismatiki Katoliki ni mkondo wa neema ya kufanya hai ule usharika au urafiki wa Roho Mtakatifu unaotuunganisha na Yesu kama wana pamoja naye kwa ajili ya waumini wote Walei-wa kike na kiume, Watawa, Mapadre, Maaskofu na kita mtu katika Kanisa."*Neema ya Bwana wetu Yesu Kristu na Upendo wa Mungu Baba na Ushirika wa Roho Mtakatifu viwe nasi sote, sasa na hata milele. Amina*"

## 1. 3 MALENGO YA KJLRISMATIKI KATOLIKI.

Katika tamko rasmi lililotolewa na Kanisa 21/9/1993 kuidhinisha Karismatiki Katoliki ulimwenguni kote na kuidhinisha *Statutes* (Sheria) za chombo ilichokabidhiwa na Kanisa kazi ya kulea mkondo huu yaani, ICCRS, *International Catholic Charismatic Renewal Services*, Roma imesisitiza kwamba Malengo ya Karismatiki Katoliki ni yale yale ya Kanisa lenyewe yaani:

1. Kuwasadia Wakatoliki kuonja huo ubatizo katika Roho Mtakatifu yaani kuonja kwa namna ya binafsi upendo va Mungu kwa kupokea wokovu anaotupatia kwa njia ya Mwanae wa pekee ambaye ndiye Bwana pekee na Mwokozi wetu.
2. Kuwasaidia Wakatoliki kuwa wazi kwa kupokea na kutumia karama za Roho Mtakatifu. Hizi zimeshatolewa tayari kwa njia ya Ubatizo na Kipaimara. Lakini hazijatumiwa, Ni kama vile zimelala ndani ya muumini. Ubatizo katika Roho Mtakatifu huziamsha na kumwezesha muumini kuwa hai katika kuzitumia.

3. Kuwasaidia Wakatoliki kupata maonjo na utamu ulioko katika sala za peke peke na za vikundi. Karismatiki Katoliki imeamsha katika wanakanisa ari ya sala za Kusifu, Kushukuru, Kuabudu na kujiachia katika maongozi ya Mungu. Pia mkondo huu umewawezesha Wakatoliki kutambua umuhimu wa sala ya maombezi yaliyojawa imani na matokeo yake. Muumini anatambua kwamba yeye kama mwana wa Mungu pamoja na Yesu anasali pamoja na Yesu kwa njia mbili tofauti. Kama mwana anakuwa na sala ya Kusifu, Kuabudu, Kushukuru na kujiachia kabisa kwa utii mikononi mwa Baba. Lakini kama Mchungaji, au Padre, au daraja kati ya watu na Baba anakuwa na sala ya maombezi kwa ajili ya watu wote. Anakuwa na uchungu juu ya jinsi uumbaji ulivyo mbali na Baba kutokana na dhambi. Anakuwa na ari ya kutakatifuza uumbaji kwa njia ya sala za maombezi.

4. Kuchochea Uinjilishaji Mpya. Kuinjilisha kumekuweko daima katika Kanisa. Ndio uhai wa Kanisa, ndilo tengo mahususi la Kanisa na ndicho kitambulisho cha uwepo wa Kanisa. Lakini kwa njia ya Karismatiki Katoliki kumekuweko na Uinjilishaji mpya uliojawa na ujasiri mpya, nia mpya na namna mpya zinazoambatana na miujiza ya kuthibitisha neno linalohubiriwa.

5. Kuhimiza kwa Wakatoliki malezi endelevu ya utakatifu kwa kuoanisha maisha ya Karama na maisha yote ya Sakramenti, liturujia ya Kanisa, utajiri wa mapokeo ya Kanisa na mipango yote ya kichungaji kwa Kanisa la ulimwengu na kwa Makanisa mahalia.

Kama inavyoonekana wazi, haya ndiyo Malengo ya uwepo wa Kanisa. Ndiyo pia Malengo ya Karismatiki Katoliki. Ni wazi kwamba Karismatiki Katoliki sio mkondo nje ya Kanisa Katoliki. Ni Kanisa lenyewe katika mkondo wake kama Jumuiya iliyo hai.

## 1. 4 HISTORIA YA KARISMATIKI KATOLIKI

"Amsha maajabu yako ya Pentekoste wakati huu wetu" Hayo ni maneno ya Baba Mtakatifu Yohane wa XXIII katika sala yake ya kuandaa Mtaguso wa Piti wa Vatikani. Ameongea juu ya Pentekoste mpya wakati wetu. Alitamka maneno hayo mwezi wa September mwaka 1959 katika sala ya kuombea Mtaguso wa piti wa Vatikani ambao aliutangaza rasmi wakati huo. Lakini alitumia maneno hayo hayo tarehe 26/4/1959 wakati akimtaja Sista Elena Guerra mwenye heri wake wa kwanza katika utawala wake. Alimsemea hivi "Ujumbe wa Elena ni wa wakati wote. Sote tunatambua hitaji kubwa la mmiminiko wa kudumu wa Roho Mtakatifu kama Pentekoste mpya itakayofanya upya uso wa nchi': }e, inaweza kufikiriwa kwamba Papa huyo aliitisha Mtaguso wa pili wa Vatikani ili kuliongoza Kanisa kuifikia hiyo Pentekoste Mpya? Njozi ya Papa ilikuwa kuwepo na Pentekoste mpya, kurudisha umoja wa Kanisa, na kufanya upya jamii yote ya kimataifa. Papa alipata njozi hiyo wapi? Hebu turudi nyuma.

## 1. 5. 1 SR. ELENA GUERRA (23. 6. 1835 -11. 4. 1914),

Sr. Elena ambaye anajulikana kama"Mtume wa Roho Mtakatifu" au "Mtakatifu wa Upyaisho wa Uso wa Nchi" kwa wakati wake aliuombea kimya kimya Mtaguso wa Vatikani wa Kwanza 1869-1871. Alisononeka, alifanya kazi, alisali, alifunga, aliteseka maisha yake yote kwa ajili ya "mafanikio ya Kanisa katika jitihada zake za kuunganisha Ndugu waliojitenga, ili kwa njia ya umoja huo, uso wa nchi ufanywe upya. "

Sr. Elena alizaliwa Lucca Italia 23/6/1835 na kubatizwa siku hiyo hiyo. Alilelewa vizuri sana na wazazi wake waliokuwa watu wa imani kubwa na ukamilifu wa tabia. Kutoka kwa mama yake Elena alijifunza kuwa na ibada ya pekee kwa Roho Mtakatifu na hii alifanya maisha yake yote. Miaka 1857-1871 Elena akiwa na miaka 29 baada ya kuugua kwa miaka nane, alianzisha kikundi Cha "Marafiki wa Kirohoi" kwa ajili ya kuishi mawosia ya Injili na kusaidia katika kufundisha dini mashuleni, kusambaza maandiko Matakatifu na kujihusisha na matatizo ya Kanisa kwa wakati wao. Aliwahimiza hao marafiki wa kiroho kusali kuliombea Kanisa lililokuwa linateswa sana wakati huo wa Papa Pius IX na kuombea Mtaguso wa Vatikani wa kwanza uliyofunguliwa 1869 kila siku hadi ulipofungwa 1871. Hii ilikuwa hatua ya ujasiri mkubwa sana kwa wakati wake maana ni utume wa walei ambao haukuwa umewaziwa wakati huo, hata na Kanisa lenyewe.

Tarehe 27/4/1871 Elena alihamasisha wale marafiki wa kiroho pamoja na wasichana washirika wa Bikira Maria na kuanza kile kilichoitwa "Waabudu wa siku za Usoni" Hili ni kama Shirika la" Watawa Watafakari': Aliita

Waabudu wa Siku za Usoni kwa sababu hakuwa amepata njozi ya uhakika ni mkondo gani hilo shirika litachukua. Hata hivyo Elena alijisikia kwa hakika kabisa kwamba majitoleo yake yalikuwa ya mtawa halisi. Haikumchukua muda mrefu wakati Elena alipotambua kwamba Wito wake sio wa "Mtawa Mtafakari" bali wa mtawa wa sala na kazi, hasa kazi ya kufunda wasichana. Alianzisha Shirika la Watawa na kuliweka chini ya Ulinzi wa Bikira Maria wa chumba cha juu (Pentekoste), Mt. Yoseph na Mt. Zita ambaye ni msimamizi wa Lucca. Ni wakati alipokuwa Mama Mkuu wa Shirika hili alipopata mafunuo mbali mbali ya kinabii kwa ajili ya Kanisa.

## 1. 5. 2 SR. ELENA GUERRA NA PAPA LEO XIII (1878-1903)'

Mwaka 1886 Sista Elena alifunuliwa kinabii na kuelekezwa kwamba amwandikie Baba mtakatifu na kumhimza achukue hatua mathubuti ili kufanya upya Kanisa kwa njia ya Roho Mtakatifu ambaye ndiye Roho na Moyo wa Kanisa na kwa hivyo chimbuko la kitla upyaisho. Alipouliza ushauri kwa mtu mwenye mamlaka naye alikatishwa tamaa akiambiwa "Hii ni hatua ya kijasiri mno Pengine ni ishara ya majivuno': Kwa utii aliacha kuchukua hatua hiyo. Wazo alilokuwa ameandika ni: "Baba Mtakatifu, kutokana na upendo wako, tafadhali fanya haraka kuwaita waumini waende kwenye chumba cha orofani (kama wakati wa maandalizi ya Pentekoste) ili kwa sala ya pamoja kwa umoja, ambayo daima husikilizwa mbinguni, waweze kumwita Mtakatifuzaji wa roho afanye upya uso wa

nchi': Baada ya Elena kukataliwa na mshauri wake aliachilia yote mikononi mwake yeye aliyempa huo unabii.

Baada ya miaka karibu nane, Novemba 1893, Herminia Giogetti, mtumishi wa jikoni wa watawa wa Mama Elena alifunuliwa kinabii kwamba amwambie mama Elena atekeleze unabii aliofunuliwa hapo awali. Sr. Elena hakuweza kukaa tena kimya. Hata hivyo aliondoa mashaka yake kwa kupata ushauri wa Msgr. Volpi ambaye ni mshauri mzoefu wa roho. Hatimaye alimwandikia Baba Mtakatifu kama alivyokuwa ameelekezwa. Barua ya kwanza ilipelekwa 17/4/1895. Papa Leo XIII alipokea huo ufunuo kwa moyo mkunjufu na mara akatoa agizo liitwalo "*Provida Matris Charitate*" la kusali Novena ya Roho Mtakatifu kabla ya Pentekoste katika makanisa yote duniani. Baada ya kupokea barua ya tatu ya Sr. Elena Papa leo XIII alitoa barua ya kitume iitwayo "*Divinum Illud Munus*" (Zawadi ile ya Kimungu) 17/4/1897 ambayo ni barua ya Kipapa yenye kina kikubwa mno katika mafundisho kumhusu Roho Mtakatifu. Mwaka huo huo Mama Elena alianzisha vikundi vya sala vilivyoitwa "Cenacle"(chumba cha orofani) kwa heshima ya Roho Mtakatifu. **Ndoto yake kwa ajili ya Kanisa ni kuwa na vikundi vya sala vya aina hiyo kwa kudumu katika Kanisa.** (Je, vikundi vya sala vya Karismatiki Katoliki vinahusianaje na hiyo ndoto ya Sista Elena? Tutavifanyaje ili viweze kutimiza hiyo taswira. Roho Mtakatifu aliyokua amemfunulia Sista Elena, yaani Vikundi vya kudumu katika sala za pamoja kwa umoja kama wale waliokuwa wanamngoja Roho Mtakatifu kule Orofani?)

Baada ya kugundua kwamba Maaskofu hawakujali agizo la Baba Mtakatifu kama Sr. Elena alivyofunuliwa, Baba Mtakatifu aliandika barua kwa maaskofu wote akiambatanisha nakala ingine ya ile barua ya Kitume na kusisitiza kwamba ni lazima maaskofu watekeleze mafundisho ya hiyo barua. (*Obligatory*).

Tarehe 15/10/1900 Sr. Elena alifunuliwa kwamba amdokezee Papa kuiweka wakfu Karne ya ishirini kwa Roho Mtakatifu kwa kuliongoza Kanisa lisali ile sala ya Njoo Roho Mtakatifu Muumbaji "*Veni Creator Spiritus*" usiku wa 31/12/1900 yaani kuamkia 1901 mwanzo wa Karne ya ishirini. Papa alitolea Misa Takatifu na kukaribisha Karne ya ishirini kwa kumwalika Roho Mtakatifu.

Kwa bahati usiku huo huo Mchungaji wa Kilutheri Charles Parham katika mji wa Topeka Kansas Marekani alikuwa anasali na Agnes Ozman kumwombea apate miminiko jipya la Roho Mtakatifu. Matokeo yalikuwa kama yale ya Pentekoste. Siku hii ndiyo inayodhaniwa kuwa ni mwanzo wa Dhehebu la Pentekoste, kwani Walutheri wenzake walipokataa kupokea tukio la ubatizo katika Roho Mtakatifu walimtenga. Alipoona ametengwa alianzisha hilo Dhehebu ambalo kutokana na msisitizo wa Ubatizo katika Roho Mtakatifu limekuja kujiita Dhehebu la Pentekoste. Imetokeaje Baba Mtakatifu amwalike Roho Mtakatifu akiongoza Ibada ya misa takatifu katika Kanisa Katoliki na badala yake Roho Mtakatifu

ajidhihirishe kwa Kanisa la Kilutheri? Na inakuwaje kwamba hata alipojidhihirisha kwa Kanisa la Kilutheri halikumpokea? Na ni kwa nini inakuwa lazima kuanza Dhehebu la Kipentekoste ambalo halikuwako ili Roho Mtakatifu ajidhihirishe katika Kanisa? Haya ni maswali ya kufikiria kwa makini. Na sio hayo tu. Kwa nini Kanisa Katoliki baada ya jitihada zote za Sr. Elena na papa Leo XIII limeshupaa bado kupokea huo unabii wa kumruhsu Roho Mtakatifu Aliongoze Kanisa? Ikumbukwe kwamba unabii wa Sr. Elena, mawasiliano yake kwa Kanisa kupitia kwa papa Leo XIII ni kufanya Kanisa lote la ulimwengu liwe na vikundi vya sala kama kile kikundi kilichojiandaa kwa Pentekoste kule orofani yaani kumkaribisha Roho Mtakatifu afanye kazi kwa karibu na wanakanisa kama wakati wa Kanisa la Mitume. Baada ya hatua zote hizi, Sr. Elena alipata ufunuo kwamba Maaskofu po pote duniani hawakujali maelekezo ya Baba Mtakatifu. walitekeleza ile novena ule mwaka mmoja tu na hata hawakujali kujifunza ile barua ya kipapa juu ya Roho Mtakatifu kama Papa alivyokuwa ameagiza.

Sr. Elena alifurahishwa sana na Papa alipowaandikia tena maaskofu wote ulimwenguni 18/4/1902 na kusisitiza upya agizo lake kwamba ni lazima waweke maanani ile Barua ya Kitume "Zawadi ile ya Kimungu" Hata hivyo ushupavu wa Maaskofu ulibaki. Ni swali kwamba kwa nini msukunno huo wa kuliweka Kanisa liongozwe zaidi na Roho Mtakatifu haukufuatwa baada ya kifo cha Papa Leo XIII 20/7/1903 na baada ya kifo cha Sr. Elena 11/4/1914?

Tuangalie kwa kifupi kilichotokea baada ya kifo cha Papa Leo XIII na kile cha Sista Elena Guerra. Tutapitia kwa haraka vipindi vya Mapapa waliofuata baada ya Papa Leo XIII.

**1. 5. 3 PAPA PIUS X (1903-1914).**

1. Huyu Papa alipokalia kiti cha Mt. Petro alipambana vikali na Wakala wa Shetani wanaoitwa Free Masons. Lakini zaidi sana muda wake mwingi alitumia kukabili mashambulizi ya Ufaransa. Serikali ya Ufaransa ilipitisha sheria kutaifisha mali yote ya Kanisa katika kila Taasisi na Parokia Sheria hiyo iliyopitishwa na Bunge inaitwa "Associations Culturelles'.

2. Papa huyu pia alikabiliana na mashambulizi ya Walutheri wa Ujerumani ambao walidhani kwamba Papa aliwashutumu katika barua yake ya Kipapa, "*Editae Saepe*" ya 24/5/1910. Papa alikuwa amewahimiza watu kufuata mfano wa Charles Borromeo katika kutafuta upyaisho wa kweli na sio.wa kuwadanganya watu na kuwaongoza kwenye uwanja wa kumkana Mungu. Walutheri walidhani kwamba aliongea juu yao na kuanza madhulumu makati ya Papa.

3. Uhispania pia ilielekeza madhulumu dhidi ya Kanisa tangu wakati Mfalme Karlos alipouawa 1908 kimapinduzi. Ilikuwa kama ile ya Ufaransa. Mali yote ya Kanisa ilitaifishwa.

4. Kotekote maovu yalijikusanya matishio ya vita vikuu, tamaa kubwa ya madaraka, wivu wa mataifa, na

ile dhambi ya ubahiti. Papa huyru aliyakabili kwa unyofu na utakatifu wa Kristu.

5. *Modernism* (Usasa): Watu waliotaka kutengeneza dini kuendana na matashi yao na mabadiliko ya nyakati zao. Papa aliona hatari katika hilo na akalikabili kwa nguvu zake zote.

## 1. 5. 4 PAPA BENEDIKTI XV (1914-1922).

Karibu muda wote Papa Benedikti wa kumi na tano alipokuwa katika kiti cha Mt. Petro alishughulika na usuluhishi wa mataifa katika vita vikuu vya kwanza vya dunia. Kazi yake ilikuwa ya mafanikio makubwa hivyo kwamba Uholanzi na Uingereza walikiri kwamba nafasi ya Papa katika kutafuta amani duniani ni muhimu mno. Walipeleka mabalozi wao katika Vatikani. Nchi nyingine zilifuata mfano Finland, Poland, Czechoslovakia, na Latvia. Hata Japan ilifanya vivyo hivyo. Alifanikiwa kwa juhudi zake kufanya Vatikani itambulikane kama mahali pa kuleta upatanisho.

## 1. 5. 5 PAPA PIUS XI (1922-1939)

1. Alishughulikia suala la muda ule unaopita kabla ya.-kumchagua Papa mwingine. Ilikuwa ni siku kumi na yeye akaongeza hadi kumi na tano au kumi na nane.
2. Alishughulikia pia mali ya Kanisa iliyokuwa inaingiliwa na dota katika nchi mbali mbali.
3. Amekabili wale waliosia mbegu za kukana ulimwengu wa Roho na kuzingatia tu ulimwengu unaoshikika-Wafaransa.

4. Italia ilimhuzunisha Papa kwa kuendeleza uhasama kati ya Kanisa na Serikali na kutaka Kanisa lisiwe na mamlaka juu ya siasa wakati nchi nyingine nyingi zilishakiri nafasi ya Papa. Swali hiti lilimalizika kwa mkataba wa Lateran 11/2/1929 ambapo Vatikani ilitambulikana na serikali ya Italia kuwa na mamlaka kama nchi inayojitegemea.

5. Suala la kumkana Mungu na Dini. Hiti lilitapakaa mahali pengi lakini Papa katika mapambano yake alisisitiza kitakachoamua mambo ya hatima ya wanadamu, siasa, uchumi, tauhidi, sayansi na sanaa ni imani kwamba Mungu yuko."Kuamini kwamba kuna Mungu ndio msingi usiotikiswa wa muundo wa jamii'.

### 1. 5. 6 PAPA PIUS XII (1939-1958).

1. Kazi kubwa aliyofanya Papa huyu ni kudumisha amani duniani. Alichukua nafasi kumwandikia kila mkuu wa nchi na kumsihi kutafuta na kudumisha amani.

2. Alifanya mawasiliano mengi sana ili kuepusha vita vikuu vya dunia bila mafanikio. Na hata baada ya vita kuanza aliendelea kila siku kupigania amani na baada ya vita kuhimiza kuweka misingi ya kudumisha amani.

### l. 5. 7 PAPA YOHANE XXIII (1958-1963).

1. Alichaguliwa wakati kulipokuwa na utulivu na uelewano kiasi kikubwa ulimwenwi.

2. Alipochaguliwa mara moja alitahadharisha kwamba ni lazima madirisha yafunguliwe kwani hewa imekuwa

nzito mno kwenye Kanisa. Alikuwa anazungumza kwa mafumbo kumhusu Roho Mtakatifu.

3. January 25, 1959 Papa Yohane alitangaza njozi ya kuitisha Mtaguso wa Piti wa Vatikani. Hii ilikuwa ni wiki chache tu baadayakuchaguliwakuwa Baba Mtakatifu na akazungumzia tengo lake kuwa ni "*Aggiornamento* (kufanya upya Kanisa kuendana na mabadiliko mbali. Mbali na kutathmini uttune wake).

4. Kati ya Makardianali wanne aliowateua kuwa wasimamizi (*moderators*) wa huo Mtaguso ni Kardinali Suenens ambaye alijulikana sana kwa msimamo wake juu ya Roho Mtakatifu na hitaji kubwa la kuamsha upya Karama zake katika Kanisa.

5. Katika barua yake ya kuhimiza huo Mtaguso 6/1/1962 alielezea Mtaguso kwamba utakidhi Epifania Mpya iliyongojewa, sio na Wakatoliki tu bali na watu wote, na pia kwamba Kanisa lilikuwa kwenye ulingo wa nyakati mpya.

6. Katika sala yake ya kuombea Mtaguso Papa Yohane aliomba kuweko na Pentekoste Mpya.

7. Kulikuwa na mjadala mkubwa juu ya Karama za Roho Mtakatifu na kwa bahati nzuri Mtaguso ulizungumzia kwa kirefu na kuweka katika vifungu viwili kwenye Hati juu ya Kanisa (*Lumen Gentium*) No. 4 na No. 12.

8. Matokeo ya hiyo Pentekoste Mpya hayakuonekana mara moja wala wakati wa Mtaguso wenyewe wala mara moja baadaye. Ila miaka miwili baadaye.

### 1. 5. 8 PAPA PAULO VI (1963-1978).

1. Mara baada ya kuchaguliwa aliahidi kuendelea na Mtaguso wa Pili wa Vatikani.

2. Wakati wake kikundi cha kwanza cha Karismatiki Katoliki kilianza 18/2/1967 katika Chuo Kikuu cha Duquesne.

3. Kwa muda mfupi sana vikundi vya aina hiyo vilienea pote duniani bila kuwa na mwanzilishi maalm, lakini vyote vikiwa na utaratibu unaofanana wa kusali.

4 Mwaka 1973 kulikuwa na Mkutano wa kwanza wa viongozi wa mkondo huu wa Karismatiki na Papa aliuelezea mkondo huu watu wanavutwa kuwa na sala za kina na za tafakari, wanakazia sala za masifu, wanakuwa na ukarimu mkubwa wa kutoa huduma, kuna upendo mkubwa kwa Maandiko Matakatifu, na upendo kwa jirani. Kutokana na hayo yote kama alivyosema Papa kuna dhihirisho kubwa la uwepo wa Roho Mtakatifu.

5. Mwaka uliofuata wakati Sinodi ya Maaskofu ilipofunguliwa Roma Papa kwa mara ya kwanza alizungumzia hadharani juu ya mmiminiko wa karama za Roho Mtakatifu katika mkondo wa Karismatiki Katoliki ambazo zinalifanya Kanisa liwe na hali ya ujana wakati wote. Kwa njia ya Roho Mtakatifu Kanisa linakuwa na maajabu ya Pentekoste ya kudumu.

6. Tabia muhimu ya mkondo huu kama Papa alivyokazia ni moyo wa matazamio, wa usikivu na wa unyenyekevu kwa Roho Mtakatifu. Kama alivyofanya Mama Maria na Mitume tunapaswa kujua namna ya kumngojea na kumwita Roho Mtakatifu.

7. Katika Mkutano wa Pili wa Viongozi wa Karismatiki Katoliki 1975 Papa Paulo VI alisisitiza kwamba mkondo wa . Karismatiki Katoliki sio mkondo

nje ya Kanisa lenyewe. Ni Kanisa lenyewe likiwa katika mkondo wake wa Upyatisho.

8. Papa huyu alisisitiza kwamba kwa asili yake tukio la Pentekoste ni la kudumu. Tukio la Pentekoste, maajabu ya Pentekoste, mmiminiko wa karama wakati wa Pentekoste vilifungamanishwa na Kanisa hivyo kwamba palipo na Kanisa papo hapo pana Pentekoste. Huu upyaisho wa kanisa ni nafasi ya pekee kwa Kanisa na kwa ulimwengu. Nafasi kama hizi hazipashwi kuruhusiwa zitelezee mbali, alisema Papa.

9. Papa alitambua mwamsho huu mpya na mchemko huu mpya wa Karama kutokana na Karismatiki Katoliki na yeye kama Mchungaji Mkuu na Halifa wa Petro ametoa vigezo vitatu vya kuzipima hizo Karama

* Ni lazima Karama'zilingane na mafundisho ya kweli ya Kanisa
* Vipaji vyote vya kiroho ni budi vipokelewe kwa shukurani Karama kama za unabii na ndimi zithaminiwe. Lakini orodha ya Karama katika barua za Mt. Paulo sio kamili. Haikuwa nia ya Mt. Paulo kuorodhesha Karama zote katika barua, zake. Pia Karama hizi hazitolewi kwa manufaa ya mtu binafsi bali kwa Kanisa.
* Msisitizo wa Karama ya upendo Upendo ndio utimilifu wa Karama zote.

10. Papa angefurahishwa sana kama waumini wote wangejazwa furaha ya pentekoste. Hii ina maana kama wote wangekuwa wana karama.

11. Tunaishi kipindi cha upendeleo mkubwa wa Roho Mtakatifu. Kila mahali watu wanajaribu kumfahamu zaidi kuendana na ufunuo wa Maandiko Matakatifu wanafurahi kujiweka chini ya uvuvio wake

wanajikusanya kwa msukumo wake na wanataka kuongozwa naye. Nia mahususi ya maongozi hayo ni katika uinjilishaji.

12. Wakati wake Papa Paulo VI Ofisi ilifunguliwa Roma iitwayo ICCRO (*International Catholic Charismatic Renewal Office*) kwa ajili ya kuratibisha Karismatiki Katoliki katika Kanisa la ulimwengu. Lakini bado hakukuwa na mwongozo mahususi uliokubaliwa na Kanisa wa kutoa utume maalum kwa hizo Ofisi.

**1.5.9 PAPA YOHANE PAUL0 11978 kwa siku 33 tu**.

**1. 5. 10 PAPA YOHANE PAULO II 1978**.

Papa huyu aliendelea na msimamo ule ule wa mtangulizi wake kuhusu Karismatiki Katoliki. Haya ni mahimizo mbali mbali aliyotoa kwa wakati tofauti.

1. Karismatiki Katoliki ni mapinduzi ya imani. Badala ya imani ya kiakili ambayo tumeshikilia kwa muda mrefu katika Kanisa, Karismatiki Katoliki inafufua ndani ya Kanisa uhai wa imani. Ni wazi kabisa kwamba imani ni kitu cha kiakili na moyo, lakini namna inavyodhihirishwa kwa nje kama sasa kwenye Karismatiki Katoliki kilikuwa kinakosekana. Papa ametoa ushuhuda wake mwenyewe akisema "mimi nilikua daima sehemu ya huu Upyaisho wa Roho Mtakatifu maisha yanw yote'Lnimwenw unahitaji huu utendaji wa Roho Mtakatifu. (11/12/1979 alipokea wasimamizi wa Ofisi ya kimataifa ya kusimamia huu mkondo wa Upyaisho. Kati ya hao-waliopokelewa ambayo walikuwa wanasimamia huu mkorido ni Mwadhama Suenens Cardinal Leo Joseph Askofu

Mkuu wa Bruxels Ubelgiji. Huyu alikuwa kwa muda mrefu sana mlezi wa huu mkondo na hata katika Mtaguo wa Pili wa Vatikani alikuwa mmqa wa Washawi Wakuu Wanne (*Moderators*).

2. Upyaisho wa Roho Mtakatifu utakuwa wa kweli na wa kuleta matunda katika Kanisa sio kutokana na mfilmuko wa Karama za ajabu ajabu bali kutokana na ule uwezekano wa kulea taratibu namba kubwa iwezekanavyo ya waumini kwa kadiri wanavyosa6ri kiimani katika njia zao mbali mbali za maisha ili kufanya jitihada ya unyenyekevu, ya subira, na ya kudumu kufahamu zaidifumbola Kristu na kutoa ushuhuda mzuri ztidi wa maisha. (Aliwaambia Maaskofu wa Kiitaliano alipowapokea 23/11/1980).

3. Akizunwmza na viongozi wa Karismatiki Katoliki katika Mkutano wao 4/5/1981 Papa alisisitiza nafasi ya Mapadre katika Karismatiki Katoliki."Mapadre katika Kanisa wamepewa Kipaji cha Daraja kama washiriki katika kazi ya Uchungaji ya Maaskofu. Ni washiriki wa Maaskofu katika Upadre na utume wa Yesu Kristo..... Kwa hiyo Padre anayo nafasi ya pekee isiyoachika kwa kulea Karismatiki Katoliki na jamii yote ya Kikristu. Nafasi yake sio ya upinzani au ya kwenda sambamba kwa wito halali wa walei. Kutokana na umoja wa Kisakramenti na Askofu.... Anasaidia kuhakikisha kwamba kuna uoanisho kati ya Upyaisho wa kiroho, Utume wa Walei, maisha ya Sakramenti na Liturjia ya Kanisa. Hii ndio maana tunasali,'tujalie sisi tunaolishwa mwili na damu ya Mwanao tlazwe na Roho wako Mtakatifu ili tuwe mwili mmoja na roho moja katika Kristu'(sala ya Ekaristi ya tatu"). Bila kuwa na moyo wazi kwa huu Upyaisho unaojengwa juu ya tamanio la

kukua katika mapaji ya Roho Mtakatifu analoshiriki na kita muumini kwa ubatizo, Padre hawezi kutoa utumishi wake kwa Karismatiki Katoliki.

4. Watawa wanaojiunga na Vikundi vya Karismatiki Katoliki hawapaswi kulegeza mfungamano wao wa Karama ya Kitawa, au kulegea katika utii kwa viongozi wao halali. (Papa Yohane Paulo II akizungumza na Maaskofu wa Ufaransa 16/12/1982).

5. Mwaka 1984 Papa aliwakumbusha Viongozi wa Karismatiki Katoliki juu ya wito wa Kanisa wa Uinjilishaji katika Makanisa mahalia. Upyaisho umegundua upya umuhimu wa maisha ya Sakramenti. Papa amesisitiza uhusiano mkubwa ulioko kati ya Neno la Mungu na Masakramenti. Kumtafuta Mungu kuwapaswa kuonekana katika mkabala binafsi na Bwana katika Kanisa ambalo kwa njia ya Roho Mtakatifu ndilo hasa Sakramenti ya wokovu. Katika kusherehekea Pentekoste tunamkuta Maria katikati ya Mitume. Yeye ndiye aliyepokea zawadi kubwa ya Roho Mtakatifu uhai wa Yesu. Maria ambaye ni Mama wa Kanisa anapashwa kuwa Mama na mfano wa Upyaisho katika Kani£a, (Mkutano wa viongozi wa Karismatiki Katoliki 30/4/1084).

6. Katika wakati wake alimteua Askofu Mkuu Paul Cordes makamu wa Raisi wa Baraza la Kipapa la Walei kuwa kiungo kati ya Ofisi ya ICCRO na Vatikani na pia mlezi wa huu mkondo wa Karismatiki Katoilki ulimwenguni. Kabla ya hapo Cardinal Suenens alikuwa mlezi na msemaji mkuu wa mkondo huu wa Karismatiki Katoliki tangu mwanzo. Wakati huo huo kwa kuwa Karismatiki Katoliki haikuwa na mwanzilishi, hao

walezi waliandaa mwongozo wa ulezi wao ili uongozi wa Juu wa Kanisa kule Roma utambue rasmi huu mkondo na chombo cha kuulea.

7. Tarehe 15/5/1987 Papa alisema kwa washiriki wa Mkutano wa sita wa Kimataifa wa Karismatiki Katoliki, "Nguvu  na matundaya uamshohuo, (Karismatiki Katoliki) unathibitisha kuna uhakika wa uwezo wenye nguvu wa Roho Mtakatifu katika miaka hii inayofuatia Mtaguso wa Piti wa Vatikani. Ni wazi, Roho Mtakatifu ameliongoza Kanisa katika kila enzi akilijalia vipaji vya aina mbali mbali kwa waamini. Shukurani kwa Roho Mtakatifu, Kanisa limedumu kuchipua na kuwa hai. Na upyaisho wa Roho Mtakatifu (Karismatiki Katoliki) ni kitu kilicho wazi cha uhai huo leo, ni uthibitisho wa nguvu wa kile roho mtakatifu akiambiacho kanisa (Ufu. 2:7), kwa jinsi tunavyokaribia kuhitimisha millennia ya pili."

8. Tarehe 14/9/1993 Baraza la Kipapa la Walei limetoa Tamko Rasmi la kutambua utumishi wa kuratibisha Karismatiki Katoliki ulimwenguni. Ile ofisi iliyokuwa inaratibisha huko Roma kwa jina la ICCRO imegeuzwa kuwa ni ICCRS (*International catholic charismatic Renewal Services*). Pamoja na Tamko hilo Baraza hilo limepitisha Sheria (*Statutes*) za kutambua Karismatiki Katoliki pamoja na huduma ya chombo cha kulea mkondo huo."Baraza la Kipapa la walei linatamka rasmi kutambuliwa ICCRS kama chama cha kuinua Karismatiki Katoliki ikiwa na haki za kisheria, kadiri ya Kanuni 116, ikikubali sheria zao, kama ziJivyotolewa, na kuhifadhiwa katika hazina ya hapa Makao Makuu." Imetiwa sahihi na Eduardo Card. Pironio (Rais)

na Pauli.Cordes (Makamu wa Rais) Vatican 14 September 1993, siku kuu ya Utukufu wa Msalaba.

**1. 5. 10 MUHUTASARI KWA SEHEMU HII**.

Mpaka sasa Karismatiki Katoliki imekwisha kuenea kila mahali duniani. Mwaka 1995 katika Semina maalum ya iliyofanyika huko St. Giovan Rotondo huko Italia walikuweko wawakilishi kutoka mataifa 80. Idadi ya Wanakarismatiki ulimwenguni kwa sasa ni zaidi ya milioni mia moja (100, 000, 000). Wako Walei wa kiume na wa kike, Watawa wakiume na wa kike, Mapadre, Maaskofu, Makardinali na kama alivyotoa ushuhuda wake mwenyewe, Baba Mtakatifu Yohane Paulo II ni Mwanakarama. (Mwanakarismatiki).
Amesema, "Nimekuwa daima'Mwanakarama...Ninaweza kuelewa umuhimu wa hizo Karama mbali mbali. Wote ni sehemu ya utajiri wake Bwana. Ulimwengu wa leo una hitaji kubwa la utendaji wa Roho Mtakatifu.'" Akizungumza na Baraza Ia Karismatiki Katoliki ulimwenguni 11/12/1979).

Hiyo idadi ya wanakarama milioni mia moja ni kati ya Wakatoliki milioni mia nane ulimwenguni. Ina maana wanakarama kwa sasa ni asilimia kumi na mbili na nusu.

Kwa Tanzania kuna wanakarama zaidi ya elfu kumi hivi waliotapakaa katika majimbo 22 kati ya majimbo 3o yaliyoko. Majimbo ambayo Maaskofu ameshakumbatia kwa dhati mkondo'wa Karismatiki Katoliki ni Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Moshi na Tanga. (Tangu iandikwe historia hii miaka karibu 7 iliyopita hadi mwaka huu

2015 idadi hii imekwishaongezeka). Majimbo hayo yote yana padre mlezi wa Karismatiki kijimbo pamoja na Kamati ya Huduma za
Kijimbo. Kitaifa kuna Kamati ya Huduma za Kitaifa.

Matumaini ya siku za usoni ni kwamba waumini zaidi na zaidi watazidi kujinasua na uhasi wa michanganyo na kuishi Ukristu ulio hai. Wazidi kujitoa kwa Yesu kama Bwana na Mwokozi wao. Pia majimbo zaidi na zaidi ambayo ni Kanisa mahalia yatazidi kuukumbatia mkondo huu ambao ni Roho Mtakatifu mwenyewe ameanzisha kwa ajili ya kuamsha, kuhuisha na kusimamia na. kuliongoza Kanisa lote na kumshuhudia Kristu kwa njia zilizo hai zaidi. Pia kutokana na himizo la uongozi wa juu kabisa wa Kanisa na sheria zilizopitishwa na Vatikani kwa ajili ya kulea Karismatiki Katoliki Makanisa Mahalia, yaani majimbo yatakuja kusikia sauti hii ya Roho Mtakatifu kwenye Kanisa kwani "*Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hiti ambalo Roho ayaambia Makanisa*" Ufu. 2: 7, 11, 17, 29; 3: 6, 13, na 22). Sio bila sababu kwamba Roho anarudia himizo hiti mara saba.

# SEHEMU YA PILL

## HISTORIA YA UPYAISHO WA KIKARISMATIKI KATOLIKI

(catholic charismatic Renewal)

## KULE ILIKOANZIA NA ILIVYOINGLA TANZANIA

Na Mwandishi wettt Benedict Mwakyanj ala

## ILIVYOKUWA MWANZONI

Mwamko huu wa Kikarismatiki siyo kama Uamsho wa aina nyingine katika K¢nisa au }amii kwani haukupangwa uanzeje au niseme vizuri kuwa hakukuwa na watu walioupanga kabla, kwa maneno mengine mwamko huu hauna mwanzilishi. Ni tofauti na mwamko mwingine katika Kanisa ambapo mtu alisikia wito wa Mungu wa kufanya jambo fulani katika Kanisa. Mfano mzuri ni Mtakatifu Franzisco wa Assisi aliyeambiwa na Bwana "Jenga tena Kanisa langu" na toka hapo tunajua kilichofuata.

Ilikuwa ni Februari, mwaka 1967, miaka karibu miwili toka Mtaguso mkuu wa Vatikani II umalizike ukiwa na mambo mengi ambayo yameleta mabadiliko makubwa katika Kanisa. Kabla ya mwezi huu wa pili yaani majira ya mimea kuchipua mwaka 1966, wahadhiri wawili walei katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki Duquesne (tamka Dukeni) ambacho kiko chini ya mapadri wa Shirika la Roho Mtakatifu (hebu fikiria!) walikuwa wakijihusisha na shughuli mbalimbali za kitume, kiroho na kiliturjia.

Walikata tamaa mara kwa mara walipoona juhudi zao hazikufanikiwa sana kama walivyotarajia, kwani waliona kuwa licha ya utaalamu wao katika mambo mbalimbali hawakuweza kutangaza Injili kwa nguvu kama ilivyokuwa kwa Kanisa la mwanzo kama inavyoonekana katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Wakakubaliana kuombeana kila siku ili kita mmoja ajazwe na nguvu za Roho Mtakatifu na kujaliwa Karama za Roho Mtakatifu. Hivyo walisali sala ambayo pia ni wimbo mashuhuri katika misa ya pentekoste, wimbo wa kumwalika Roho Mtakatifu, yaani SEKWENSIA.

Hawa watu wawili waliendelea kudumu katika sala hiyo kwa mwaka ule wote. Licha ya watu hawa, wengine wawili (Maparofesa, walei pia), kutoka chuo hicho, waliona upungufu huo, pasipo kuwasiliana na hao wengine, wao waliamua kwenda kuhusiana na madhehebu mengine ambayo yalikuwa tayari na vikundi vya kikarismatiki (Waanglikana na Wapresbiteri, bila shaka na Wapentekoste), nao'wakapata kile kinachojulikana kama Ubatizo katika Roho Mtakatifu.

Hapo Chuoni kulikuwa na kikundi cha kujiosomea Biblia (Chi-Rho), katika maandalizi ya Kwaresima ya mwaka 1967, walipanga kuwa na mafungo mwezi Februari, na wakawaomba hao wawili waandae mafungo hayo ya Mwisho wa wiki hapo chuoni. Ili kujiandaa kwa mafungo wanafunzi na washiriki wengine wa mafungo walipewa kazi za kufanya ili kusaidia tafakari, kazi hiyo ilikuwa ni kujisomea kitabu cha Matendo ya Mitume na kitabu cha "the Cross and the Switchblade" cha Mchungaji David Wilkerson, (Kitabu hiki kimetafsiriwa

kwa Kiswahili kinaitwa "Wahuni waliobadilika" na kinapatikana katika maduka mengi ya vitabu vya dini hapa Tanzania). Kitabu cha Wilkerson kiliwashangaza wengi wao na kuwagusa sana hasa anaposimulia kwamba aliweza kuzungumza na Roho Mtakatifu naye ahmwambia jambo fulani la kutenda na kwa kweli jinsi alivyohusiana na Roho Mtakatifu ilikuwa inashangaza, jambo hiti linakubaliana na sehemu za kitabu cha Matendo ya Mitume ambapo Roho Mtakatifu anaagiza jambo fulani lifanyike au lisifanyike, hebu tazama Mdo 20:17-23.

Siku ya Jumamosi jioni ilikuwa ni siku ya mapumziko mchana waliitumia kwa sala, na ilikuwa pia ni siku kuu ya kuzaliwa padri mmoja hapo Chuoni. Kutokana na mguso huo mara tu baada ya kula na bila kuwasiliana na mwingine wanafunzi wawili wakaenda kwa Ralph Keifer ili awaombee ili na wao waweze kupata kile ambacho walikuwa wamesikia muda mrefu yaani Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mwanafunzi mwingine Patti Ghallagher yeye aliamua kwenda kwenye Kikanisa cha pale Chuoni na huko aliuhisi uwepo wa Roho kwa namna ya pekee kwa mshangao mkubwa aliamua kwenda kuwaita wenzake na wengine bila kuitwa waliamua kwenda huko Kanisani. Mmoja nmioja kati ya wanafumzi na wahadhiri walianza kujisikia msukumo ndani yao na kwenda mara moja katika Kanisa la hapo Chuoni ili kumwomba Mungu awamwagie Karama hizo za Roho Mtakatifu.

Wakati huo Patti alikuwa amesharudi Kanisani na kukaa kwa muda mbele ya Ekaristi Takatifu na kumwomba

Mungu, na mara akajikuta anaendelea na furaha ile ya ajabu na hali ya uwepo mkubwa wa Mungu kujidhihirisha, akajikuta analala kifudifudi mbele ya Ekaristi katika hali )ra kuabudu. Mara mwingine naye akaja Kanisani na baada ya muda akajikuta machozi yanamtoka bila ya yeye mwenywe kujua kwa nini analia, huku amenyosha mikono juu na kumwomba Mungu.

Mara wengine wakaongezeka na pasipo kutegemea na pasipo mwaliko rasmi wale waliokuwa wanahudhuria mafungo wakajikuta Kanisani, wengine wamelala kifudifudi, mwingine yuko kimya, mwingine analia na zaidi ya yote wengine humo humo Kanisani wakaanza kunena kwa lugha ngeni na hii kwao ilidhihirisha uwepo wa Munw kati yao kwa namna ya pekee, furaha na amani vilitawala mahali pale. Kati yao hakuna aliyejua nini kitafuata baada za hapo au kudhani kwamba huo ndio ulikuwa mwanzo mdogo kabisa wa mwamko ambao utagusa maisha ya Wakatoliki wengi pote duniani; waliendelea katika hali hii toka saa nne usiku hadi saa kumi alfajiri.

## USHUHUDA WA PATTI GALLAGHER

Patti, niliyemtaja hapo juu, anaeleza hivi juu ya kile alichoking'amua siku ile:
"Usiku ule tarehe 18 Februari, 1967 Bwana alikileta kikundi chote mle Kanisani. Nikajikuta sala zangu zikibubujika kumwomba Bwana awajalie wengine kumfahamu (Kristu)... wale Maprofesa wakaweka mikono yao juu ya baadhi ya wanafunzi, wengine wetu

tulipokea Ubatizo katika Roho tukiwa tumepiga magoti mbele ya Ekaristi Takatifu, tukiwa katika hall ya sala. Wengine wetu tulianza kunena kwa lugha, wengine walipokea karama za kupambanua Roho, unabii na hekima. Lakini kubwa kuliko zote ni ile ya Upendo ambayo ilikiunganisha kikundi chote".
Kwa sababu jambo hiti lilitokea kwenye Chuo Kikuu tena cha Kikatoliki habari zake hazikusambaa mitaani mara moja, kwani ilihusisha wanafunzi, maprofesa na wahadhiri wengine maarufu ila mara moja zilisambaa kwenye Chuo kingine maarufu cha Kikatoliki cha Notre Dame huko huko Marekani, na baadaye kwenye Chuo Kikuu cha Iowa na kile cha Michigan na kile cha Portland (Oregon). Lakini mchango mkubwa uliofanya moto huu usambae kwa kasi namna hii, ni pale ulipofika Chuo Kikuu cha Notre Dame. Hapa nielezee kile kilichotokea Chuo Kikuu cha Notre Dame hasa baada ya habari za mwamko huu zilipofika.

## MOTO UNAWASHWA

Watu karibu 20 walikutana katika nyrumba ya Kelvin na Dorothy Ranaghan siku ya Jumamosi Machi 4, 1967. Kelvin alikuwa anajiandaa kupata Shahada yake ya Udaktari wa Falsafa katika Teolojia hususani upande wa Liturjia. Kama wengine kwenye kikundi yeye pia alijihusisha katika mwamko wa kiliturjia pale Chuoni. Walikuwa wamekutana hasa kwa Mkutano wa Sala na wakati huo rafiki yao mmoja alikuwa amelika hapo mjini na wakaona ni vizuri kumwalika kwenye huo Mkutano wa Sala. Huyo alikuwa ni mmoja wa Maprofesa wa Chuo Kikuu cha Duquesne na Kelvin alikuwa ni mmoja

wa wanafunzi wa huyo Profesa huko nyuma, na alihusika sana kwenye matukio ya usiku ule wa mafungo kule Duquesne. Habari za yaliyotokea huko zilikwisha fika Notre Dame ama kwa kupigiana simu au kwa kutembeleana na hivyo ilikuwa pia ni hayo.

Mkutano ulianza kwa kusoma Waraka wa kwanza wa Paulo kwa Wakorintho sura ya 14 ambapo anazungumza juu ya Karama ya unabii na lugha. Baada ya watu kadhaa kuchangia maoni yao juu ya kifungu hicho, ndipo
huyu mgeni naye alipopewa nafasi ya kusema juu ya yale yaliyotokea huko Duquesne na mtazamo wake. Alieleza kwa kirefu juu ya maandilizi ya mafungo ya Duquesne na jinsi watu walivyojikuta wamevutwa kwenda Kanisani na yale yaliyowakuta huko akasema kuwa matokeo ya usiku ule yalikuwa ni ya kushangaza sana kwani maisha ya kiroho ya wanafunzi wengi yaliamshwa kwa upya, kwani wengine walishapoteza Imani na siku' hiyo Imani yao ilichochewa na wengi wakaamua kdmfanya Kristu kweli awe kitovu cha maisha yao. Na wengine wakajikuta wamepata nguvu ya kuwaeleza wengine kwao Kristu alikuwa wa maana gani. Akasema kuwa Karama zilizokuwa katika Kanisa la mwanzo zilionekana tena hasa Karama ya lugha ngeni na baada ya maelezo mengi alihitimisha kwa kusema kuwa "Mimi siamini tena habari ya Pentekoste, nimeiona mwenyewe!" Watu waliokutana kwenye nyumba ya Ranaghan walishangazwa sana na profesa huyu, walivyomfahamu mwanzoni na jinsi alivyozungumza juu ya Ubwana wa Yesu na nguvu ya Mungu ilikuwa inashangaza sana. Watu wengine wanazungumza mambo

hayo kitaaluma mno na kutumia misamiati ya ajabu lakini hapo yupo mtu ambaye anazungumza mambo hayo kwa urahisi mno ni kama mtu aliyejiamini na kujua kile anachoongea. Yeye mwenyewe alikuwa ni ushahidi wazi kwani wengi walimfahamu kabla ya hapo.

Siku iliyofuata kukawa na Mkutano nyumbani kwa Bert Ghezzi. Alipata shahada yake ya juu huko Duquene na alikuwa Notre Dame kwa ajili ya Shahada ya Udaktari wa Falsafa katika Historia. Watu wengine tisa pamoja na mgeni walikuwapo hapo, wengi wao walikuwepo jana yake kwenye nyumba ya Kelvin. Baada ya mazungumzo na nyimbo na kusoma neno wakamwomba huyu mgeni awawekee mikono ili na wao wapate neema hiyo ya Pentekoste. Ingawa Ndugu huyu alikataa mwanzoni kwa kusema kuwa yeye hakuwa na uwezo wa kugawa Karama hizo, baadaye hata hivyo alikubali kuwaombea. Hakuna jambo la ajabu lililotokea siku hiyo.
Baadaye mmoja wao alileta habari kuwa kuna mtu mmoja aitwae Ray Bullard anafahamu mambo mengi juu ya Karama na wakampigia simu aje ili aweze kuwasaidia katika mambo hayo. Wiki iliyofuatia wakaalikwa kwa ajili ya Mkutano wa Sala nyumbani kwake (Ray). Wakati huo Ray alikuwa ni kiongozi wa Full Gospel Businessmen Fellowship na mshiriki wa Kanisa la Assemblies of God. Ray alikuwa na hofu ya kukutana na hawa "Wasomi" wa Kikatoliki. Hivyo alikaribisha viongozi wengine wa Kipentekoste ili kujibu hoja zao nzito. Mmoja wa Wachungaji hao alitoa somo juu ya Karama za Roho na mwingine alijibu maswali. Baadaye Wapentekoste hao wapatao 20 waliwazunguka wageni wao na kuanza kuwaombea. Kwanza waliomba kwa

lugha wao wenyewe na baada ya dakika chache, nane kati ya watu tisa walioombewa walianza nao kunena kwa lugha ngeni. Kwa dakika 25 waliendelea katika hali hiyo na baadaye wakaendelea na majadiliano yao juu ya Karama. Hiyo ilikuwa ni tarehe 13 Machi, 1967.

Mkutano wa kwanza wa Sala wa Kikarismatiki ulifanyika siku chache baadaye njrumbnai kwa Dr. Kelvin Ranaghan, ukihudhuriwa na watu wapatao 20 hivi. Kati yao walikuwepo toka Chuo cha Maria Mtakatifu na Mapadri wawili kati yao ni Padre Edward 0'Connor, Profesa wa Theolojia katika Chuo Kikuu cha Notre Dame. Ilipofika tarehe 14 April, 1967 Mikutano ya Sala ilifanyika mara kwa mara na sasa idadi ya wanakikundi ilifikia 200. Wakati wote huo taarifa ilishatolewa kwa askofu Leo A.Pursley wa Jimbo la Fort Wayne ambaye hakukataza au kukubali moja kwa moja. Alisema itabidi asubiri kutoa uamuzi hadi atakapowasiliana na Askofu mwingine, ila alisisitiza kuwa "hali hiyo inahitaji Karama nyingine kupambanua nyingine." Siku hiyo ya tarehe 14, baada ya kama saa moja hivi Kusifu na Kuabudu, mtu mmoja alisimama kati ya kundi na kusema "Mimi siyo Mpentekoste na hata simuamini Roho Mtakatifu, nimekuja tu kuangalia kile kinachofanyika, mimi ni mwanasaikolojia, lakini vyo vyote vile kile kinachofanyika ni kizuri'.

Mikutano iliendelea, kufanyika watu wakiendelea kuombewa Ubatizo katika Roho Mtakatifu na wengi walikuta maisha yakibadilishwa na ilikuwa wakati huu pia kukawa na haja ya kuwa na uongozi. Viongozi

wakaanza kupatikana polepole. Wale waliohitimu katika Vyuo Vikuu nilivyovitaja hapo na walikuwa wakijihusisha na mwamko huu hapo Chuoni walirudi katika nchi zao na kueneza mwamko huu huko kwao kama Uingereza, Ireland, Australia na New Zeland na nchi nyingine.pia kama Ufaransa, Ubelgiji, Ujerumani na nyingine zilifikiwa na mwamko huo. Na pasipo kuchelewa mwamko ukawa umeingia Italia na hususani katika mji wa Roma.

## MIKUTANO YA KIMATAIIA

Kuanzia mwaka 1 968 mikutano ikaanza kufanywka kwenye Chuo Kikuu cha Notre Dame, kwanza ikiwa ya Kitaifa na baada ya muda mfupi ikawa ya Kimataifa, ikikusanya maelfu ya watu kwenye viwanja na katika mikutano hii adhimisho la Ekaristi lilikuwa la kipekee, watu maelfu kwa maelfu wakiimba na kucheza mbele za Bwana. Mwaka 1971 watu 4500 walihudhuria kati yao ni Mapadri 147 na Askofu Stephen na Askofu Joseph McKinney waliongoza misa. Mwaka 1972 watu wapatao 11, 000 walihudhuria toka nchi 16. Mwaka 1973 kiasi cha watu 22, 000 walihudhuria, hadi ikabidi Kongamano lifanyike kwenye uwanja wa mpira wa miguu. Kati yao walikuwepo Mapadri 500. Misa iliongozwa na Askofu Mkuu James Hayes na Kardinali Suenens kutoka Malines Ubelgiji ambaye alitoa mahubiri. Mwaka 1975 mikutano hii ikaanza kufanyika Roma. Tarehe 19 May, 1975 kwenye Mkutano huo wa Roma siku moja tu baada ya Pentekoste Wakarismatiki wapatao 10, 000 waliadhimisha Misa pamoja na Kardinali Suenens.

Ilitarajiwa kwamba Papa mwenyewe alitoa ruhusa kwa Kardinali Suenens kutumia Altare ambayo hutumiwa na Papa mwenyewe. Baadaye Papa mwenywe alitokea na kutoa hotuba kwa Wakarismatiki ambayo iliamsha shangwe, vigelegele ndani ya Kanisa hili kubwa la Mt. Petro na watu kuimba kwa lugha ngeni. Nitaeleza baadaye juu ya kile alichokisema Papa.

Hivyo basi unaweza kuona mwanzo finyu wa mwamko huu na jinsi ulivyokua haraka. Hivi sasa ni miaka 45 toka Uamsho huu uanze kwenye Kanisa Katoliki, na umekuwa ni mwamko mkubwa kabisa ulioanzia chini labda toka ule wa Kifransiskani wa karne ya 13. Kuenea kwake kuliwashangaza watu wengi, umefika ambako hakukuwa na dalili na umegusa maisha ya watu na kuyabadilisha pasipo kufikiria. Katika kusambaa kwake mwamko huu umefika Tanzania. Hebu basi nikusimulie kile kilichotokea Tanzania na hadi kufanya mwamko huu utokee.

## MWAMKO WA KIKARISMATIKI WAINGIA TANZANIA

Kwa kweli ni vigumu kuonyesha kikundi cha kwanza cha sala kilianzia wapi kwani kuna ushahidi wa kutosha kuonyesha kuwa hadi kufikia tarehe 7/12/1980 kulikuwa na vikundi nane ambavyo Wakatoliki walijihusisha navyo. Vingi kati ya hivyo vilikuwa vikihudhuriwa na Mapadri na Watawa. Hii inawezekana bila shaka ni kwa sababu wamisionari wengi waliokwenda likizo kati ya mwaka 1970 na 1974 huko U1aya walikutana na wimbi la mwamko huu ulioletwa na Roho Mtakatifu. Baadhi

yao baada ya kurudi wakaanza kukutana kwa sala za Kikarismatiki. Walei wachache walishiriki katika vikundi hivi na sehemu nyingine Askofu aliruhusu Mapadre na Masista wakutane wenyewe.

LUKULEDI-MASASI Kilianza wakati wa kipindi cha Kwaresma mwaka 1980 kikiongozwa na Padri Roman Stadmueller.

DAREDA-BABATI-Kikundi kilianza mwishoni mwa mwaka 1979 chini ya Masista wa M.M.M. (*Medical Missionaries of Mary*).

BIGWA-MORO GORO-Miongoni mwa vikundi vya zamani zaidi kilianza mwaka 1976 hivi na wahusika walikuwa Wakatoliki waliojishughlisha na Unitas.
TANGA-Vikundi vilianzishwa mwaka 1978 kwa wale wanaozungumza Kiingereza tu na kile cha wale wanaozungumza Kiswahili.

MOSHI-Masista kadhaa wakibatizwa katika Roho wakiwa U1aya au Marekani kwa likizo au masomo, hivyo kati yao walikuwa na Vikundi vya Sala kama kile chl Masista wa Kifransiskani wa Maua Moshi.

MWANZA-Kulikuwa na Kikundi cha Sala kwa muda mrefu chini ya padre Hector Almeida S. J. lakini kikafa baadaye.

DAR ES SALAAM-Kikundi kilianza Chuo Kikuu na Wapentekoste lakini Wakatoliki kadhaa walijihusisha

kati yao ni Masista wawili ingawa baadaye waliondolewa shirikani kwa sababu hiyo.

MBEYA Kikundi kilianza mwaka 1974, lakini Askofu alikataza kuendelea na mambo hayo hadi mwaka 1980. Askofu hakuweka kikwazo kikubwa na watu walianza kukutana tena chini ya Padri Etienne Sion M.Afr.

Hivyo basi vilikuwa vikundi vichache ambavyo vilianza peke yake peke yake kila kimoja na hivyo inakuwa vigumu kupata historia yake vizuri kwani sehemu nyingine vikundi vimekufa baada ya kuondolewa wawakilishi, sehemu nyingine Maparoko walivipiga marufuku n. k. Lakini pamoja na hayo vikundi vingine vinaendelea na kukomaa kwa karibu ya miaka 20 au zaidi.

## HAJA YA KUKUTANA YAJITOKEZA

Padri Etienne Sion M. Afr. aliingia nchini mwaka 1968 akitokea Ufaransa mara tu baada ya Upadrisho wake. Na moja kwa moja alipangiwa kuanza huduma ya kichungaji huko Mbeya. Mwaka 1971 alipata nafasi ya kwenda kusoma zaidi huko Ireland na zaidi juu ya shughuli za Ekumene. Akiwa huko Ireland alikutana na Wakristo Wakatoliki na wa Madhehebu mengine katika kozi yao. Karibu na mahali walipokuwa wakisoma kulikuwa na Kikundi cha Kikarismatiki lakini si cha Kikatoliki bali cha madhehebu mengine. Watu kadhaa kutoka Chuoni walikuwa wakihudhuria hivyo naye kutokana na masomo aliyokuwa akichukua akaona vyema jioni moja aende na wengine kwenye kikundi

hicho ili naye aweze kuombewa kwa ajili ya Ubatizo katika Roho Mtakatifu. Alienda na Kushiriki kwanza Mkutano wa Sala ingawa namna ya kueleza mambo mbalimbali na mtindo wa sala ulivyokuwa haukumvuta sana lakini aligundua kuwa kuna kitu cha Mungu hivyo alikubali kuwekewa mikono na Walei na Wakristu wengine waliokuwepo. Hakunena kwa lugha au jambo lolote la kipekee halikuonekana kwa nje, lakini kama anavyosimulia mwenyewe kulikuwa na mabadiliko Fulani aliyoyaona

## HISTORIA YA PADRE ETIENNE SION

Mara alipomaliza masomo yake na kupata Shahada ya juu alirudi nchini kwenye huduma ya Parokia na hivyo akaanzisha kikundi, hiyo ilikuwa ni mwaka 1974. Baada ya kuzuiliwa na Askofu kuwa na Kikundi cha Sala, aliruhusiwa kuendelea na huduma ya kupunga pepo na kuombea wagonjwa huko huko Parokiani kwake. Mwaka 1980 Askofu hakumzuia tena na hivyo akaendela kuongoza'watu wengine kwenye kikundi (walikuwa wanakutana yeye na Masista kadhaa). Hapo ndipo ilipojitokeza haja ya kutaka kuwakutanisha wale wanaojishughulisha na mwamko wa Kikarismatiki na hasa Mapadri na Watawa ili waweze kuona wanaweza kufanya nini kwa Karismatiki humu nchini.

Mwanzo mkutano ulifikiriwa ufanyike Mbeya lakini haikuwezekana, hivyo alimwomba Askofu Adriani Mkoba wa Jimbo la Morogoro (sasa ni marehemu) aruhusu mkutano ufanyike Jimboni mwake. Ingawa lengo lilikuwa ni kuwakusanya viongozi wa Makanisa

mbali mbali ya Kikristu na kujadiliana juu ya mwamko wa kiroho katika Afrika Mashariki, Askofu Mkoba akaonelea ni bora wakusanywe Wakatoliki tu labda na Waanglikana wachache.

Basi baada ya mawasiliano kati ya Padre Etienne na viongozi wa Karismatiki huko Brussels Ubelgiji. Na baada ya kutuma barua katika Parokia mbalimbali_hapa nchini ili kutoa mwaliko kwa Mapadri na Watawa ambao wangependa Kushiriki mkutano huo majibu yalikuja toka kwa viongozi wapatao 150 na hivyo maandaJizi yiliendelea.

Alipoandika barua kwenda Brussels Ubelgiji kuelezea nia ya kuwakutanisha Viongozi, padri Etienne alitaja sababu tatu :

1. Vikundi vingi vya Tanzania vilihudhuriwa na Mapadri wa Watawa hivyo kuna haja ya kuwakutanisha ili kwa pamoja kuweza kuweka maono yao pamoja na kutafuta hatua ya pili iwe nini.
2. Kwa sababu kulikuwa tayari na uamsho ulioanzia Uganda, na tayari umeshaingia Tanzania, na Wakatoliki kadhaa walishiriki katika mikutano hiyo ya Madhehebu mengine. Karama mbali mbali zilijidhihirisha na Wakatoliki walijiunga na vikundi hivyo, kwa hiyo haja ilikuwepo ya kuwakutanisha Viongozi wa Kanisa na kuelezea kuwa hayo yanayotokea kwenye Madhehebu mengi yameanza pia kwenye Kanisa Katoliki.
3. Kuwaelewesha Viongozi hao juu ya mambo mbalimbali yahusianayo na mwamko huu na hasa juu ya Karama za Roho Mtakatifu. Basi mkutano ulipangwa

kufanyika Morogoro· kama nilivyosema awali na ulipangwa kufanyika huko.

**MZUMBE-IDMMOROGOR0 21/09/1981**

Watu mbalimbali walioahidi kushiriki Mkutano huo walifika Morogoro kati yao ni Mapadri, Watawa na Walei. Walipata mahali pa kulala huko Bigwa kituo cha Unitas na mkutano ulifanyika kwenye Chuo cha Maendeleo Mzumbe. Mkutano ulitarajiwa kufunguliwa na Mhashamu Askofu Adrian Mkoba lakini kutokana na kwenda safari huko Roma, msaidizi wake mkuu (vicar General) Padri Thelesphory Mkude alifungua mkutano huo.

**MKUTANO WA PILI-BIGWA MEI 03/06/1982**

Mkutano wa pili wa Viongozi wa Karismatiki ulifanyika pale Bigwa na kweli uliweka historia ya Karismatiki hapa Tanzania. Ulihudhuriwa na washiriki 60 kati yao Mapadril3, Mabruda 3, Masista 18. Walikuwepo kati yao wageni kutoka Kanisa la Anglikana wakiongozwa na Askofu Graceford Chitemo na Mapadri 3 na Ndugu wengine watano. Mkutano huu ulifunguliwa na makamu wa Askofu Padri Thelesphory Mkude wa Jimbo la Morogoro.

Kwa  kweh tengo la mkutano lilikuwa ni mafungo kwa Viongozi hao wa Ka;rismatiki. Aliyetarajiwa kuongoza mafungo hayo ni Padre Fiorello Mascarehnas S. J. kutoka Romli ambaye wakati huo alikuwa ni Mkurugenzi wa Ofisi ya Kimataifa ya Karismatiki

Katoliki ICCRO (*International Catholic Charismatic Renewal Office*). Katika mafundisho yake Padre Fiorello aliwahamasisha washiriki kwa kuwaelezea hah ya Kanisa ilivyokuwa na kwa nini kuna haja ya kutokea mwamko wa kiroho ndani ya Kanisa.

Mwisho wa Mkutano huo Padri Fiorello alishauri kuunda Timu ya Huduma kwa ajili ya kuratibu shughuli za uamsho huu hapa nchini Tanzania. Wafuatao walikuwa wajumbe wa kwanza wa Timu ya Huduma hapa Tanzania:

1. Padri Donat Mueller Ofin. Cap. Toka Ifakara.
2. Sr. Catherine Mboya toka Maua Moshi
3. Ndg. Octavian Nyalusi toka Morogoro
4. Dada Perpetua Lihepa toka Morogoro
5. Padri Hector Almeida S. J. toka Dodoma
6. Padri Etienne Sion toka Mbeya
7. Dada Fortunata Pasipanofu toka Mpwapwa.

Mratibu wa kwanza alikuwa ni Padri Etienne Sion, Katibu wa kwanza alikuwa Ndugu Octavian Nyalusi (sasa ni marehemu) na mweka hazina Dada Perpetua Lihepa.

Hivyo basi toka mwaka 1981 hadi leo hii kumeendelea kuwa na Mikutano ya Viongozi Kitaifa. Na kwa miaka yote hii mwamko huu wa Kikarismatiki unaendelea kuenea katika kona mbalimbali za Tanzania. Hadi sasa kuna vikundi angalau kimoja katika majimbo 17 nayo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mahenge, Mbeya,

Morogoro, Moshi, Same, Iringa, Sumbawanga, Tanga, Zanzibar, Tabora, Mwanza, Shinyanga, Rulenge, na Kigoma. Vikundi hivi ni vya zamani kidogo lakini vingi pia vimeanza katika miaka hii ya 90. Kuna karibu parokia 55 zenye vikundi vya sala vya Kikarismatiki hapa Tanzania. Idadi ya vikundi vile vya zamani na vipya vinafikia 73. Jimbo la Mbeya likiwa na vikundi 25. Idadi ya Wakarismatiki kaaka vikundi hivi hadi hivi sasa (1997) yaweza kufikia 6, 000. Jimbo la Moshi likiwa na Wakarismatiki 970. Na bado kuna mialiko mingi kutoka katika pande mbalimbali za nchi kuanzisha vikundi hivyo na kuleta mwamko wa Kikarismaaki katika Parokia nyingi. (Tangu historia hii imeandikwa 1997 ni miaka 18 imepita na tunapoichapisha leo hii 2015 idadi ya Majimbo yenye Karismatiki Katoliki imeongezeka sana na idadi ya Wanakarismatiki imeongezeka pia).

Hivyo basi ni historia fupi ya mwamko wa Kikarismatiki ndani ya Kanisa Katoliki, sehemu mbalimbali hasa kule ulikoanzia na hapa Tanzania.Mengi yanasemwa juu ya mwamko huu. Wengine wanasema si Ukatohki, wengine wanasema ni kuchafua Kanisa, wengine wanasema ni kikundi cha'walokole ndani ya Kanisa letu. Na wengine wanasema ni kitu kizuri. Lakini wale walioko katika mwamko huu pasipo shaka wanasema kuwa wao ni Wakatoliki kabisa. Ili kuweza kutoa hukumu ya haki ni vizuri kuangalia yale yaliyomo ndani ya mwamko huu (yale yanayotendwa na kusemwa) na kutoka hapo tunaweza kuona na kuamua kwa haki. Licha ya kuangalia yaliyomo kubwa zaidi ni kuangalia matunda yaani matokeo ya, mwamko huu.